SIKU YA KIMATAIFA YA MAOMBI KWA WAATHIRIKA
WA USAFIRISHAJI HARAMU WA BINADAMU 2023

TUME YA KIMATAIFA YA HAKI ZA BINADAMU

JESHI LA WOKOVU

# NIMESIKIA VILIO VYAO



## MSAADA KWA WATU WAZIMA KUHUBIRI

Imeandikwa na **Kamishena Prema Wilfred (R)**
*Teritori ya India Kusini Magharibi*

**'Wana wa Israeli wakaugua kwa sababu ya ule utumwa, wakalia, kilio chao kikafika juu kwa Mungu kwa sababu ya ule utumwa. Mungu akasikia kuugua kwao, Mungu akakumbuka agano lake alilolifanya na Ibrahimu na Isaka na Yakobo.' (Kutoka 2:23-25).**

### UTANGULIZI

Utumwa wa kileo na usafirishaji haramu wa binadamu ni sekta ya uhalifu ya dola mabilioni mengi inayonyima uhuru watu karibu milioni 49.6 duniani kote. Hao ni wanawake, wanaume, wasichana na wavulana wanaolazimishwa kuingia katika aina mbalimbali za kazi na usafirishaji kwa ajili ya ngono na ndoa za kulazimishwa.

Duniani kote leo, Jeshi la Wokovu linasimama kwa umoja katika mapambano haya ya kupata uhuru kwa kuungana pamoja kuomba kwa ajili ya watu walioathirika na utumwa wa kileo na usafirishaji haramu wa binadamu. Tunataka kuombea wana familia walioachwa nyuma na kwa Kanisa kusimama lipambane. Tunataka kuomba upatikane mwisho wa mahitaji yanayosababisha utumwa wa kileo na usafirishaji haramu wa binadamu na kwa wasafirishaji na wanyonyaji wanaojishughulisha na kunufaika na ukosefu huu wa haki ya jamii.

Tunapojiandaa kujihusisha na maombi, tunakwenda kutazama tukio la mapema la utumwa katika maisha ya Waisraeli linalopatikana mwanzo wa kitabu cha Kutoka na hasa Kutoka 2:23-25, jinsi moyo wa Mungu ulivyo wa kuwaondoa watu watoke katika giza la utumwa waingie katika mwanga wake.

Mwanzo wa Kutoka unatusaidia kuelewa hali ambayo Waisraeli walikuwa wanaipitia wakati huo – mapambano yao, kukandamizwa kwao na utumwa huko Misri. Tunapoangalia nyuma katika historia ya Waisraeli katika nchi hii ya kigeni, tunamwona Yusufu akiuzwa utumwani na kaka zake.

Utumwa ni pale ambapo mtu humtawala mtu mwingine kama yule mtu ni kitu au ni mali yake. Utawala huo hutegemea tishio la na/au matumizi halisi ya ukatili iwe wa kimwili, kihisia, kisaikolojia, kiroho au kifedha. Wakati watu wanapitia utumwa, wananyonywa. Hii maana yake ni

kwamba wanatendewa isivyo halali kwa manufaa ya mtu mwingine.

Watu walio katika utumwa wanadhalilishwa na kutendewa kama wao ni kitu. Utu wao na uwezo wa kufanya maamuzi wananyang'anywa. Vikwazo vinawekwa kila sehemu ya maisha yao. Wanalazimishwa kutoa sadaka tumaini lao, ndoto zao, wapendwa wao, mambo yao ya nyuma na ya mbele. Kama wanalipwa kwa kazi zao, huwa sio kiwango cha kutosheleza kuishi. Huwanyang'anya uhuru wao na ni ukiukaji wa haki zao za ubinadamu.

Alipokuwa mtumwa wa Farao, Yusufu alipitia magumu mengi, uchungu na ukandamizaji. Hata hivyo Mungu alikuwa na kusudi na maisha ya Yusufu. Mungu alimkomboa Yusufu kutoka kwa mapambano yake akamwinua kufikia ngazi ya juu ya uongozi Misri. Yusufu aliwasamehe kaka zake wakati wa njaa na akawasaidia kuhamia Misri.

Baada ya Yusufu kufariki na Farao mpya akaingia madarakani, Wamisri waliwaogopa Waebrania waliokuwa wanaongezeka kwa kasi ndani ya nchi yao na kwa makusudi wakatafuta kuwaua watoto wa kiume wa Waebrania wanaozaliwa.

Lakini Mungu aliingilia kati akamwokoa Musa kwa ajili ya kusudi lake. Kuona kwamba bado Waisraeli walikuwa wanaongezeka kwa kasi kiidadi, Wamisri waliwalazimisha kufanya kazi – utumwa.

Hata kama Waisraeli walikuwa sasa raia wa Misri na walikuwa wanafanya kazi ya kujenga na kuiboresha nchi, lakini bado walikuwa hawahesabiwi kuwa binadamu na haki zao walinyang'anywa. Walikandamizwa – maisha yao yalijaa ugumu usio na haki, walikosa usawa, maumivu na uchungu. Hakuwepo mwenye uwezo wa kuzikabili nguvu za Farao au kupambana kupata haki. Kutokana na uchungu na maumivu yao, 'waliugua katika utumwa, wakamlilia Mungu' (Kutoka 2:23).

Kutoka 2:24-25 inaelezea kuhusu majibu ya Mungu kwa vilio vya watu wake. Majibu yake yanaelezwa katika maelezo matatu mafupi: alisikia kilio chao; alikumbuka agano lake; alihusika. Hebu tutizame kila moja ya majibu haya.

## MUNGU ALISIKIA VILIO VYAO

Katika tafsiri ya (New International Version), neno 'kuugua' lililotumika katika Kutoka 2:23 linaunganishwa kwa karibu na wazo la 'kulia kwa sauti'. Neno hili 'kuugua' linatumika mara tatu tu katika Agano la Kale: Kutoka 6:5, Waamuzi 2:18 na Ezekieli 30:20. Waisraeli walikuwa wanaugua na kulia kwa sauti kwa sababu ya dhiki ya kimwili iliyokuwa inasababishwa na mazingira yao ya kazi ya utumwa kwa maisha yao ya pamoja. Waebrania wakati huo hawakuwa na kiongozi – hawakuwa na wakumgeukia. Hawakuwa na uwezo wa kufanya lolote na walikuwa bila tumaini. Lile waliloweza kufanya lilikuwa kumlilia Mungu. Vilio vyao havikuenda kwa miungu ya wapagani bali vilienda kwa Mungu Muumba wa dunia hii na watu wote. Vilio hivi vilimwendea Mungu wa baba zao na Mungu alisikia vilio vyao. Katika Maandiko yote, tunajifunza namna Mungu anavyosikia vilio vya watu wake.

**1 Petro 3:12** inasema, 'Kwa kuwa macho ya Bwana huwaelekea wenye haki, na masikio yake husikiliza maombi yao, bali uso wa Bwana ni juu ya watenda mabaya.'

**Zaburi 50:15** inasema, 'ukaniite siku ya mateso, nitakuokoa na wewe utanitukuza.'

**Zaburi 34:17** inasema, 'Walilia, naye Bwana akasikia, akawaponya na taabu zao zote.' Vifungu hivi maalum vya Maandiko na vingine vingi vinatwambia kwamba Mungu wetu husikia vilio vya watu wake. Alisikia vilio vya Hajiri jangwani na vilio vya wengi wengine. Alikutana na Hajiri na wengine wakati wao mgumu na akawaokoa. Mungu yule yule anasikia vilio vya watu wote wanaopitia katika utumwa. Moyo wake ni wa kusikiliza na kukutana nao mahali walipo.

## MUNGU ALIKUMBUKA AGANO LAKE

Mungu sio tu alisikia bali alikumbuka au alifikiria kuhusu agano alilolifanya na Ibrahimu, Isaka na Yakobo (Kutoka 2:24). Neno 'alikumbuka' katika Kiebrania ni 'Zakar', ambacho ni kiini muhimu cha theolojia katika kitabu cha Kutoka. Katika Kiebrania, kukumbuka sio tu zoezi la kiakili lakini ni pamoja na kuifanyia kazi hiyo kumbukumbu. Mungu alikuwa amefanya ahadi zisizo na masharti na Ibrahimu na vizazi vyake. Sio kama wanadamu, Mungu ni mwaminifu. Yeye hasahau ahadi alizozitoa. Atazikamilisha hata kama inaonekana kwetu inachukua muda mrefu kufanya hivyo. Nyimbo hizi nzuri, 'wakati wake, hufanya vyote kuwa vizuri wakati wake' inatukumbusha kwamba wakati wake ukiwadia, yeye huwakumbuka watoto wake. Hasahau. Zaburi 105:8 inachangia kusema kwamba 'Hukumbuka agano lake daima, ahadi alizotoa, kwa vizazi maelfu'. Yeye huwakumbuka watoto wake kizazi hadi kizazi. Huwakumbuka wale wote wanaoteseka na wanapitia utumwa. Mungu ni Mungu anayewakomboa watu kutoka kwa utumwa wowote na kuleta uhuru kamili wa wokovu.

## MUNGU ALIHUSIKA

Mungu sio tu alisikia kuugua na vilio vya Waisraeli na akakumbuka agano lake, lakini alihusika vile vile kuhusu wana wa Israeli. Mungu wa Israeli hakuwa mjinga wa hali mbaya ya watu wake au hakutaka kuwaokoa kutokana na utumwa. Alikuwa anapanga kufanya jambo ili awaokoe kutokana na utumwa waliokuwa wanapitia Misri. Vitendo hivi vya kusikia, kukumbuka na kuhusika vilikuwa ishara ya uaminifu wake na huruma zake kwa uumbaji wake.

Kama isemavyo katika Zaburi 146:6-9, 'Aliyezifanya mbingu na nchi, bahari na vyote vilivyomo. Huishika kweli milele, huwafanyia hukumu walioonewa, huwapa wenye njaa chakula, Bwana hufungua waliofungwa; Bwana huwafumbua macho waliopofuka; Bwana huwainua walioinama; Bwana huwapenda wenye haki; Bwana huwahifadhi wageni; Huwategemeza yatima na mjane; bali njia ya wasio haki huipotosha.'

Tunapoelekea katika muda wa maombi na kupitia katika vituo vyetu vya maombi, siwezi kusisitiza vya kutosha kwamba tunaposoma mwanzo wa Kutoka na kuelekea kwenye Kutoka 2:23-25 Mungu haidhinishi utumwa, usafirishaji haramu wa binadamu na unyonyaji. Mungu wetu ni Mungu anayesikia, anayekumbuka, naye anahusika na watu wote wanaopitia kunyimwa haki hii. Kila mmoja aliumbwa kwa mfano wake naye ameumbwa awe huru katika hali zote. Moyo wake ni wa kuwatoa watu watoke kwenye giza la kunyimwa haki hizi na awalete kwenye mwanga wake. Hebu tuchukue muda tuombe tunapozunguka katika kituo cha maombi tukiutafuta moyo wake na majibu yake kwa wale wote wanaopitia utumwa, usafirishaji haramu wa binadamu na unyanyasaji.

---

"**Huwakumbuka** wale wote wanaoteseka na kupitia katika utumwa. Mungu ni Mungu **Anayewakomboa** watu kutoka kwenye utumwa'